# NGURUMO ya MWANDISHI

Toleo LA VII-Aprili-MMXXII



## Usikate Tamaa

# USIKATE TAMAA

KUKATA tamaa ni dhambi. Wengi wanasema hivyo. Na kwa kuwa tunaamini kuwa sauti ya wengi ni sauti ya Mungu, basi kukata tamaa ni dhambi.

Katika pitapita yangu huku na huko nimegundua kuwa watu wengi; wake kwa waume wamekata tamaa katika mambo mbalimbali, lakini wote ni kwa sababu hawajapata kile walichokitamani. Na mbaya zaidi ni kwa kuwa mtu amefanya juhudi nyingi sana lakini hajafanikiwa na wakati huohuo mwingine wala hajatumia nguvu, akafanikiwa. Inauma ujue! Halafu inakatisha tamaa.

Je; wewe umeshawahi kukata tamaa katika jambo fulani?

Tatizo la kukata tamaa hupelekea maafa makubwa kwa baadhi ya watu hata kufikia kukatisha maisha yao ama kwa kujinyonga au kumeza vidonge vingi na hata kunywa sumu. Usifike huko! Hutakiwi kufika huko. Na kwanini ufike huko?

Siri kubwa ya kuupita huo mtihani ni kutokukata tamaa. Unatakiwa ufanye yafuatayo ili uvuke kihunzi hicho.

1– Usijifananishe na mwingine. Katika utafutaji kila mmoja ana mbinu na uwezo wake. Usimtazame bali panga mbinu mpya ya ushindi.

2– Amini unaweza kuliko Yule aliyepata. Jifunze zaidi katika hilo na anza upya. Usiseme 'sizitaki mbichi hizi'.

3-Uvumilivu… anza na kidogo kadiri ya nguvu yako. Taratibu utaweza kukifikia kile kikubwa utakacho.

Kamwe mmea hauwezi kukua kwa kuvutwa kwenda juu, bali kumwagiwa maji na kutiwa mbolea. Furahia Jarida lako! ***RM***

## SERIKALI YAMWAGA NEEMA KWA WAANDISHI WA RIWAYA

Na: Mwandishi wetu

**WAZIRI MKENDA ATOA FURSA KWA WAANDISHI WA VITABU NCHINI**

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda (Mb) amesema Wizara itatenga bajeti kwa ajili ya mtu yeyote mwenye muswada wa kuandika riwaya ambazo zitashindanishwa na muswada ambao utashinda utagharamiwa uchapishaji wake na Wizara.

Amesema hayo Jijini Dodoma alipokutana na wawakilishi wa Mwandishi wa Kitabu cha Hesabu kilichoandikwa kwa kutumia mitaala ya Kenya, Uganda na Tanzania, David Inzofu ambapo amesema lengo ni kuona kunakuwa na Watanzania wengi wanaojitokeza kuandika vitabu.

Waziri Mkenda amemuagiza Kamishna wa Elimu kuhakikisha kitabu hicho kinapitiwa na wataalamu kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) ili kama kuna sehemu ya kuboresha iweze kuboreshwa kwa lengo la kumsaidia mwandishi huyo ili kuongeza hamasa kwa Watanzania wengi zaidi kuandika



vitabu na kuhamasisha usomaji.

"Tunataka kusaidia waandishi ambao wanataka kuandika riwaya. Tunaposema elimu yetu tunataka iakisi mahitaji ya nchi yetu na utamaduni wetu tungependa pamoja na wanafunzi kusoma vitabu vya nje wasome pia vilivyoandikwa na Watanzania," amesema Prof. Mkenda. Amesema kumekuwepo na maoni ya kutumia Kiswahili kufundishia katika siku zijazo, hivyo kunahitaji maandalizi ili kuweza kufika huko, Watanzania wenyewe waandike vitabu wawe tayari, uwezo na uzoefu wa kutafsiri vitabu vya Kiingereza kuwa vya Kiswahili.

"Tungependa kukuza Kiswahili na hii inahitaji maandalizi, hivyo lazima kuwe na vitabu vingi vya Kiswahili, huwezi kuanza kutumia lugha ya Kiswahili huku vitabu vikiwa vya Kiingereza. Huyu mwalimu David Inzofu nafurahi kwamba ametafsiri hiki kitabu kwa Kiswahili itabidi tumsaidie ili Baraza la Kiswahili lihakiki kitabu hicho," ameongeza Waziri Mkenda. ***N.M***

# MWANDISHI WETU: KALMAS KONZO



**Katika ukurasa wetu wa Mwandishi Wetu, Ngurumo ya Mwandishi, Toleo la VII linamtembelea Yule mnayemjua kama Inspekta Tom Green**

---

Naitwa Kalmas Konzo. Nimezaliwa Mafinga mkoani Iringa, lakini kwa sasa ninaishi mjini Njombe katika mkoa wa Njombe.
Historia yangu katika utunzi na uandishi wa hadithi imeanzia mbali sana. Wakati nikiwa mdogo nilikuwa napenda sana kusoma vitabu vya waandishi nguli kwa kipindi hicho hususani hadithi za kijasusi. Waandishi kama Aristablus Musiba, Ben Mtobwa, Hammie Rajab, John Simbamwene n.k walinijenga sana katika kupenda hadithi.
Nikiwa nasoma mimi na rafiki yangu bwana Fadhy Mtanga tulikuwa tukipeana hamasa kubwa sana katika utunzi na uandishi wa hadithi.
Tulikuwa na ndoto za kuja kuwa waandishi wakubwa hapo siku za baadaye.
Mwaka 2010 ndiyo nikaanza kutunga simulizi rasmi maana kipindi cha nyuma nilikuwa nikitunga kama sehemu ya burudani yangu.
Mpaka sasa nimefanikiwa kuchapisha kitabu kimoja kiitwacho LADHA YA KIFO. Mungu akijaalia mwishoni mwa mwaka huu nitaingiza sokoni vitabu vingine viwili.
Pia nina hadithi nyingi sana ambazo ziko katika mfumo wa nakala laini.
Instagram napatikana kama @hadithi_za_konzo na facebook napatikana kama Simulizi za Konzo.
Nawashukuru sana waandishi wenzangu wote kwani tumekuwa na ushirikiano mkubwa katika kubadilishana mawazo pamoja na kujengana.
Naawashukuru pia wapenzi wa hadithi zangu kwani siku zote wamekuwa pamoja nami na kuniunga mkono katika njia mbalimbali.
Mwisho nichukue fursa hii kuiomba jamii yote ya Watanzania kuamsha ari ya usomaji. Unaposoma, unaushibisha ubongo maarifa. Fanya vitabu kuwa ni sehemu ya bidhaa unazonunua mara kwa mara.
Ahsante sana uongozi wa jarida la NGURUMO YA MWAMNISHI kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuweza kuonekana katika ukurasa huu. Mungu awabariki na niwatie moyo kwa hiki mnachokifanya.


Penda kusoma vitabu

www.richardmwambe.com JAMVI la SIMULIZI

Faida za kusoma vitabu:

- Msisimko wa Akili
- Kupunguza Msongo wa Mawazo
- Kuongeza Ujuzi wa mambo mbalimbali
- Kuongeza Msamiati
- Huboresha Uwezo wa Kukumbuka
- Hukupa Uwezo Mkubwa wa kuchambua na kufikiri
- Huboresha Mtazamo na Umakini

**Fanya vitabu kuwa ni sehemu ya bidhaa unazonunua mara kwa mara.**

# HADITHI: USIWE MUUAJI—01



Na: JANE DAVIS

**"Hihihi oooh Baba! Kwanini umeruhusu hili? Ee Mwenyezi kimekukosea nini kiumbe chako hadi umeamua kumpa mateso makubwa namna hii?" Ilisikika sauti ya mwanamke mmoja akilia huku akiongea maneno mengi kumlaumu Muumba.**

Mama Masanja aliishi maisha ya ujane kwa takribani miaka ishirini tangu mumewe mpenzi alivyouawa na watu wasiojulikana usiku alipokuwa akitoka kilabuni.

Wakati mumewe alipouawa alimwacha mwanawe Masanja akiwa mdogo mwenye umri wa miaka saba tu. Mjane huyo hakukata tama bali alipambana kufa na kupona ili kumlea mtoto wake.

Sauti hiyo ilitokea ndani ya chumba kimoja kati ya vyumba vitatu vya nyumba chakavu iliyojaa mipasuko na nyufa nyingi ukutani. Nyumba hiyo ndimo alimokuwa akiishi mjane huyo zliyejulikana kwa jina moja tu, Mama Masanja. Katika uzazi wake, Mama Masanja alibahatika kupata mtoto mmoja tu wa kiume. Yeye na mumewe wakampa jina, Masanja.

Ujane, upweke na nguvu ya upande mmoja havikumnyima mbinu za kuishi. Alifanya kila analoweza ili mwanawe huyo aweze kupata mahitaji yake muhimu kama chakula na elimu bora.

Kila kazi aliyoona itampatia kipato aliifanya, alikuwa akiamka alfajiri kuchoma vitumbua na kuchemshia chai ambayo aliuza asubuhi maeneo ya maegesho ya magari.Mchana vilevile alirudi nyumbani akichukua chane kadhaa za ndizi na kuanza kutembea mitaani akiuza.Kipato kidogo alichopata alinunua unga Kwa mangi akakoroga uji akiutia ukwaju na pilipili manga kisha kuanzia mida ya saa moja usiku hujipanga barabarani na Wamama wengine kuuza.

Hakika hilo alifanikiwa, kwani mwanawe alifanya vizuri katika elimu yake ya msingi, sekondari, na kiwa na umri wa miaka ishirini na sita alihitimu elimu yake ya juu na kuwa mkandarasi wa kuongoza mitambo huko kwenye migodi.

Leo hii Masanja yupo kitandani,mgonjwa mahututi. Ugonjwa wake haujulikani, kwani kila kitu kimekuwa utata. Amekaa hospitali kwenye sadaruki kwa muda mrefu, Hatimaye wakaruhusiwa kwenda kumuuguza nyumbani.

Siku moja nyumba hiyo ilipokea mgeni. Si kwamba hawakumjua, la! Walimjua vyema. Hakuwa mwingine bali Bi. Stumai. Mwanamke huyu jirani yao tu, alikuwa na uwezo kifedha, ukilinganisha na Mama Masanja ni sawa na Mashariki na Maghalibi. Hawalingani.

Alimtazama Masanja, afya yake imedhoofu sana, ngozi yake imenyauka na kupoteza nuru. Bi Stumai kilio kikubwa.

"Ona jamani kamkono ona kijana alivyoisha uuuwii kwanini Baba unataka kumchukua kijana huyu mapema" Aliendelea kuongea huku akiushika mkono wa Masanja na kuupima unene kwa kushikanisha ncha za kidole chake cha kati na gumba.

Mama Masanja na mkamwanawe iliwapasa kuanza kumbembeleza mama huyo ambaye aligoma kabisa kunyamaza. Wakasaidiana na kumuinua mpaka sebuleni. Na kuketi pamoja naye. Kasha mkewe Masanja akaenelea na kazi yake ya kuandaa chakula cha mumewe

Maneno yale yalisikika vema masikioni mwa mkewe Masanja, mwanamke yule akaishia tu kuguna. Moyoni alimuomba sana Mungu isiwe hivyo alivyosema bi Stumai.

Alimpenda mno mumewe ambaye ndio kwanza imepita miezi sita u tangu wafunge ndoa kanisani. Penzi lao hawakulifaidi kwani likiwa bado la motomoto, miezi mitatu tu ya mwanzo mumewe ndipo aliugua.

Baaa ya kufuta mahozi, Bi. Stumai alifungua kinywahe, "Yaani jamani inasikitisha sana hali ya Masanja".
“Usihofu Bi. Stumai, tuombe tu Mungu yeye huwa hashindwi na jambo lolote" Aliongea mama Masanja.
********
Nini kilimpata Masanja?
Kuna heri kwa ujio wa Bi. Stumai?

***Itaendelea toleo lijalo...***

# RAFIKI BORA NI VITABU—02



Na Joshua Golyama

**Kwenye vitabu kuna kila kitu ambacho wewe unakihitaji ili kufikia ndoto zako kwa mafanikio makubwa sana.**

Unapata kuhamasika na yale ambayo yalifanyika hapo zamani yanayofanana na lile ambalo wewe unalifanya.
Unatakiwa kuambatana na Yule ambaye haamini katika kushindwa na badala yake anaamini katika kushinda. Mwenye anaona sababu lukuki za kulifanikisha lile ambalo unataka kulifanya. Naye si mwingine bali ni VITABU.

Wako marafiki wengine ambao wana mitazamo hasi, wanaamini katika kushindwa na pengine kuwa na sababu na visingizio vingi vya kutofanya au kuendelea na kile wanachokifanya.

Wanaopenda Kukata TAMAA kila wakati, Wasiotaka kujifunza kila siku, wasiotaka kukosolewa na mengine mengi.
HAWAKUFAI WATU WA AINA HII, na una kila sababu ya kuwaacha na kuchagua marafiki wengine wazuri wanaoweza kukusaidia, kukufundisha, kukuelekeza njia sahihi ya kufika kule ambako wewe unataka kufika.
Bila shaka Rafiki KITABU ndiye rafiki bora sana na ambaye kila mmoja wetu anapaswa kuomba Urafiki naye na kasha kuambatana naye kwa kila hatua ambayo tunazipiga kila siku.

Na sio KITABU tu bali KITABU SAHIHI, huyu atakusaidia sana kufika kule unakotaka kufika, huyu anakuletea story za watu mbalimbali waliotangulia ambao walifanya mambo mbalimbali, wengine walishindwa na wengine walifanikiwa sana.

Rafiki huyu atakusimulia story ya wale ambao hawakuona sababu hata moja ya kukata tamaa licha ya changamoto mbalimbali ambazo walikabiliana nazo, mfano Kukosa PESA, KUKATALIWA, ULEMAVU na zinginezo nyingi ambazo wewe unazifahamu au kuzisikia.
Bila shaka kwa kusimulia story hizi za kweli zitakuhamaisha wewe na pengine kukupa nguvu zaida kusonga mbele bila ya kukata tamaa.

Na rafiki huyu anayo orodha ya watu wengi ambao waliwahi kufanya kile ambacho wewe unatamani kukifanya, kwa kupitia kuwafahamu watu hawa utajifunza njia ambazo wao walizitumia, changamoto na mafanikio makubwa sana ambayo waliyapata.
Na utajua ni wapi pa kuanzia safari yako, milima na mabonde na namna utakavyoweza kukabiliana nayo.

Lakini rafiki huyu KITABU atakuunganisha na watu wengine wakubwa na wenye Hekima na Busara katika kufanya mambo mablimbali. Waflame, Wafanya biashara wakubwa, Bilionea na watu wenye sifa mbalimbali hapa duniani.
Anakufungulia dunia nzima na kuileta mahali ulipo, unapata nafasi ya kuyafahamu mambo mbalimbali kwa upana wake.
Bila shaka hautajuta kabisa kuwa naye maishani mwako.
This is my best friend ever to have on earth, because teaches me and direct me in the right way.
Huyu ndiye rafiki ambaye mimi rafiki yako nakuletea kwako hivi leo, tafadhali fanya urafiki naye, na kamwe hautajua kabisa kumfahamu.



Na: Joshua Golyama

**MUHIMU;** Ambatana nasi katika mtaa wetu ambako rafiki huyu ninayekusimulia habari zake kila siku anapatikana, na huku tunapiga naye *story* na hakika anatufundisha mambo mengi sana ambayo yanatufaa katika maisha yetu ya kila siku, na kutupatia MAARIFA NA UFAHAMU.
Mtaa huo unaitwa ***Street of Books*** (Mtaa wa Vitabu) huku tunayo mada moja tu ya KUJIFUNZA NA KUSOMA VITABU.

**Makala hii imeandikwa na;
Joshua Golyama
(Mwandishi, Mwalimu, Blogger na Mwazilishi wa Taasisi ya Elimu Kitaa Foundation).
Mawasiliano; +255 764 257 495/ +255 622 163 323.**

# MHALIFU ALIYEIUSUMBUA FBI KWA MIAKA THELATHINI—01

**Kutoka Maktaba**

Alijulikana kama, *The Friday Night Bank Robber.*

Ulimwengu unamshuhudia Mmarekani aliyefanikiwa zaidi kutekeleza matukio ya ujambazi akitoka gerezani baada ya kuwa jela kwa miaka kumi na saba (17) baada ya kufanikiwa kuishawishi serikali na mahakama kupunguza kifungo chake kutoka miaka mia moja kumi na tano (115) mpaka miaka hiyo kumi na saba.

Atakaporudi uraiani atakuwa na miaka sitini na tisa (69) ya kuzaliwa. Huyu si mwingine bali Carl Gugasian au maarufu kama 'The Friday Night bank robber'

Mhalifu aliyeliumiza kichwa FBI kwa miaka thelathini (30) akitekeleza matukio hamsini ya kuzivamia na kuziibia benki pasipo kukamatwa, kitendo kilicholipelekea FBI na waendesha mashitaka wa Marekani 'kumsifu' kuwa ndiye mhalifu mwenye akili na aliyefanikiwa zaidi katika historia ya nhi hiyo.

Kumekuwa na kelele nyingi kutoka kwa 'mashabiki' wakiitaka Hollywood watengeneze filamu kuhusu maisha ya 'The Friday Night Bank Robber'!

Jambo lililowashangaza wengi na ulimwengu wote ni jinsi gani binadamu mmoja aliweza kutekeleza matukio hamsini ndani ya miaka thelathini akiwa peke yake na FBI washindwe kujua hata utambulisho wake na kukosa hata mbinu ya kuweza kumzuia au kumtia nguvuni.

Mbinu, weledi na nidhamu aliyokuwa nayo na kuvitumia kutekeleza matukio yake vilijenga siri na kitendawili mpaka pale alipokamatwa na kuamua kuwasimulia makahero wa FBI ili kujaribu kuwashawishi kumpunguzia adhabu ya kifungo. Na akafanikiwa.

Hebu tumtazame Carl Gugasian ni mtu wa namna gani na majiundo ya uhalifu wake yalikuwaje!

## Nia ya kuwa mhalifu mwenye weledi mkubwa



Carl alitekeleza tukio lake la kwanza la ujambazi akiwa na miaka kumi na mitano tu, ambapo alijaribu kuiba fedha katika duka la peremende bila mafanikio na alipigwa risasi tumboni na kukamatwa. Baada ya kukamatwa alipelekwa katika jela ya watoto ya Camp Hill na kukaa huko kwa takribani miezi kumi na minane kama adhabu.

Baada ya kutoka jela Carl alidhamiria sasa kuwa ni lazima awe mhalifu mwenye weledi wa hali ya juu kiasi kwamba atafanikiwa katika kila tukio na hatoweza kukamatwa. Carl akajiapiza kuwa kama anataka kufanikiwa kuiba fedha nyingi kwa wakati mmoja basi sehemu sahihi ya kuiba ni benki. Na kama anataka kweli awe mhalifu mweledi, angetakiwa ajue namna sehemu hizo (*majengo na mifumo yake)* zinavyofanya kazi. Alitakiwa kufahamu namna ya kutumia silaha, pia ajue namna ya kujihami *(self defense)* na namna atakavyo toroka na fedha atakazoiba.

Baada ya kuweka dhamira hiyo Carl akachukua hatua ya kwanza na alichofanya ilikuwa ni kujiunga na Chuo kikuu cha Villanova ambapo alisomea uhandisi wa umeme. Akiwa chuoni hapo alitumia mwanya huo kujiunga na mafunzo maalum ya jeshi la Marekani kwa ajili ya kuwajengea ukakamavu vijana walioko vyuoni. Baada ya kumaliza chuo akaenda kutumikia jeshi kwa muda mfupi katika kituo cha Fort Bragg na huko akapata mafunzo maalumu ya kijeshi *(Special Forces and tactical weapons training)*

Baada ya kupata mafunzo ya kijeshi Carl akarudi huo kusoma Shahaa ya Uzamili ya *System Analysis* na alipomaliza shahada hiyo akafanya mafunzo ya awali kwa ajili ya Shahada ya Uzamivu katika maswala ya takwimu.

Mtaani alipokuwa akiishi alijiunga na kituo kinahofundisha sanaa ya mapigano *(Martial Arts). Hapo alijifunza mbinu za kujihami katika sanaa* ya mafunzo ya kujihami, karate na judo, ambapo alifanikiwa kupata mkanda mweusi.

***Itaendelea toleo lijalo...***

# UJIO WA JOSEPH SHALUWA KATIKA MAHUSIANO NA NDOA

**NA Richard Mwambe**

WENGI wanapasuka vichwa juu ya namna gani wanaweza kuwa kwenye uhusiano bora ambao utazaa ndoa njema hapo baadaye. Lakini pia wapo wanandoa ambao ndoa zao zinawaka moto kutokana na migogoro iliyopo ndani yake.

Makundi haya yanahitaji neno la faraja na maarifa mapya ya kuwavusha katika uhusiano wao. Mwandishi Joseph Shaluwa anatoa dozi kamili kwa makundi hayo kupitia kitabu cha MAISHA YA NDOA – Toleo Jipya ambacho kipo tayari kuingia mitaani katikati ya mwezi huu, Mei.

Akizungumza na NGURUMO YA MWANDISHI, Shaluwa ambaye ni mume wa Upendo – baba wa watoto wanne – Ben, Kelvin, Eric na Erica anasema, ameamua kutoa kitabu hiki baada ya kupata maombi ya wasomaji wengi.

"Hiki ni kitabu cha pili. Nimeshatoa kitabu cha kwanza mwaka 2014. Leo hii miaka minane baadaye, nimeamua kutoa toleo jipya. Ndani yake kuna mada mpya kabisa na chache zilizotoka katika kitabu cha kwanza, lakini nimeziboresha baada ya kufanya utafiti wa muda mrefu," anasema Joseph Shaluwa ambaye ni memba wa Umoja wa Waandishi wa Riwaya Wenye Dira Tanzania (Uwaridi).

Nilitamani kujua alianza lini uandishi na ilikuwaje wakati alipotoa kazi yake kwa mara ya kwanza. Huyu hapa anafafanua mwenyewe: "Nilianza kuandika nikiwa na umri wa miaka tisa (9) tu. Nilianza kutunga michezo ya kuigiza kanisani kwetu - *Sunday School.*

"Sikujua kama ni kipaji ambacho kingezalisha ajira hapo baadaye. Wakati nasoma shule ya upili, ndipo sasa nikaanza kuandika rasmi. Nakumbuka nilikuwa nasoma sana magazeti ya udaku wakati ule yakiuzwa Tsh. 100. Yalikuwa ni Kiu, Ijumaa, Uwazi, Sanifu, Komesha, Kasheshe, Fukuto, Risasi na mengineyo.

"Kulikuwa na simulizi nyingi ndani yake, lakini nilivutiwa zaidi na waandishi Eric Shigongo, Sultan Tamba na Amri Bawji (marehemu). Nilikuwa nasoma si tu kama burudani, lakini kujifunza zaidi kupitia wao. Nikajikuta naboresha zaidi kazi zangu.

"Nakumbuka mwaka 2004, kwa mara ya kwanza hadithi yangu iitwayo LAZIMA NIKUUE ilitoka kwenye Gazeti la Nipashe, ikafuatiwa na SAFARI YA KABURINI kwenye gazeti la Mwananchi. Ndiyo safari yangu ya uandishi ilipoanza.

"Siku ya kwanza kununua gazeti lenye kazi yangu, nilichanganyikiwa kwa furaha.

Nilijikuta natembea nalo mitaani karibu mwezi mzima, kuwaonesha watu kazi yangu," anasema Shaluwa, ambaye ni mzaliwa Singida - Mnyiramba.

Anaongeza: "Baadaye mwaka 2005, nilianza kuandikia magazeti ya Habari Corparation (sasa New Habari (2006) Ltd), kama mwandishi wa kujitegemea."

Anasema, mwaka 2006 alipata kazi katika Kampuni ya Global Publishers inayomilikiwa na Eric Shigongo (Mbunge wa Jimbo la Bushosa - CCM). Hiyo ilikuwa ni baada ya kutumikia Kampuni ya Hali Halisi Publications (HHP) kwa miezi saba (Machi – Oktoba, 2006), iliyo chini ya Saed Kubenea (aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ubungo (CHADEMA) awamu iliyopita).

Baadaye mwaka 2015 alirudi New Habari ambapo alikuwa Mhariri wa Burudani wa magazeti ya Mtanzania Weekend – matoleo ya Jumamosi na Jumapili.

"Desemba, 2018 nilirudi tena Global Publishers, kabla ya kupunguzwa kazini 2020 kutokana na janga la Korona. Lakini bado naendelea kuandika hadithi kwenye Gazeti la Championi Ijumaa, pia ni mtunzi wa simulizi za sinema fupi zinazorushwa na Global TV," anasema Shaluwa.

Ifuate Ukurasa wa 09

# MPIGA MBIO — 07



Richard Mwambe

*Inatoka toleo lililopita*

**Mara hii hata yeye alijishangaa; inakuwaje anajipeleka kwa Kenneth? Kwani Kenneth siyo mwanaume? Jakamoyo. Vita ya maamuzi moyoni mwake ilitamalaki.**

*Endelea...*

Hakupokea ile simu, badala yake aliangaza macho huku na kule na mara akashtushwa na simu nyingine. Hii ilikuwa ya Kenneth, akaipokea.

"Umeshafika mrembo?" akaulizwa. Ikunda hajawahi kuitwa 'mrembo' kwa miaka mingi sana tangu akiwa shule ya msingi. Huko alikuwa akiitwa hivyo na mwalimu wake wa darasa.

"Nimefika! Nakuja nipo hapa nje…" akajibu na ile simu ikakatika. Akiwa anairudisha kwenye mkoba wake, akagundua kuna arafa haijasomwa, akaifungua.

*'Hata ukijifanya mjanja nitakupata tu…. Mi ndiye Habibu kama umekataa ombi langu najua nitafanya nini…. utaingia tu kwenye kumi na nane zangu! Wasalimie Mlimani City'*

Ile arafa almanusura imfanye Ikunda ajikojolee. *Ameniona?* Akajiuliza. Ikunda alijikuta hana raha tena, alishindwa kujua afanye nini katika hilo. *Habibu anaweza kunifanyia kitu kibaya?* Akajiuliza zaidi. *Nimwambie Kenneth au nifanyeje! Ah mapema mno, liwalo na liwe!* Akamaliza kuzungumza na nafsi yake, akavuta hatua na kuingia ndani ya mgahawa huo tayari kukutana na yule anayeuvuruga moyo wake.

Ndani ya mgahawa ule, Kenneth aliinuka na kumlaki Ikunda. Alitoka kwenye kiti alichokalia na kumkumbatia kabla hajashtuka kuwa keshasema neno '*darling*'. Upande wa Ikunda, neno lile lilisikiwa na ngozi badala ya sikio. Liligonga mishipa midogomidogo inayosambaa mwilini ikipita kwenye moyo, mapafu, viungo vya uzazi na kuishia kwenye ubongo.

Ogopa sana ngozi yako inapopokea ujumbe wa mapenzi, tafsiri yake katika ubongo huwa ni ya nguvu na umakini kuliko ukipokewa na sikio.

Ikunda alijikuta akisisimkwa mwili kwa mambo makubwa mawili; kwanza hakuwahi kukumbatiwa na mwanaume, pili hakuwahi kuitwa *darling* tangu azaliwe. Alijikuta ghafla kafika sayari nyingine, sayari nyekundu yenye watu wenye upendo wa kweli unaotoka moyoni. Akaketi mkabala na kiti kile alichoketi Kenneth.

"Vipi? Mbona unaonekana haupo sawa, kuna kitu kinakusumbua?" Kenneth akauliza huku akimtazama Ikunda usoni. Mwanamke huyo hakuweza kustahimili, alielekeza macho yake mezani kwa soni. Hakuzowea.
"Anh anh siyo kitu…" akajibu huku akichezea simu yake ndogo aina ya *BUNDY*.
"Bibiye mpaka leo unatumia simu kama hii? Wadada wa taipu yako wanakuwa na simu wanayofanana nayo," Kenneth akamwambia.
"Una maneno wewe hata sikutegemea! Hii mi ndiyo taipu yangu hizo nyingine gharama, mi ntaweza 'api!" Ikunda akajibu, akimaanisha.

Ikunda amekuwa mtoto aliyelelewa na mama pekee kufuatia kifo cha baba yake kilichotokea miaka michache baada ya kuzaliwa kwake. Amekua katika mikono yenye shida. Yeye akiwa wa tatu na wa mwisho katika familia yake alijikuta ana jukumu kubwa la kumlea mama yake hasa katika uzee wake. Dada zake wawili walikwishaolewa na hawakuwa na msaada wa karibu kwa mama yao. Baada ya Kenneth kumdadisi kiume, mwanamke huyo alimsimulia mambo mengi ya maisha yake. Simulizi hii, ilimchoma sana Kenneth ambaye mpaka umri huo alikuwa na wazazi wote wawili. Katika maisha yake hakuwahi kupitia shida isipokuwa zile za kawaida tu.
"Nimefurahi leo kuwa pamoja na kitinda mimba!" akamtania. Ikunda akatoa tabasamu la siri lakini Kenneth aliliona na kulipokea.
"Niambie basi mi nataka kuwahi…" Ikunda akamwambja Kenneth.

***Itaendelea***

Riwaya ya

MPIGA MBIO

inatarajiwa kuwa katika mfumo wa kitabu. Weka oda yako sasa kupitia 0766974865

# ...KATIKA MAHUSIANO NA NDOA

*Inatoka ukurasa wa 07...*

*MAISHA YA NDOA NI KITABU CHA NAMNA GANI HASA?*

"Cha mahusiano – nimeandika mada za kuwajenga wote – wanaojiandaa kuingia kwenye ndoa na walio kwenye ndoa. Ambaye bado hajaingia kwenye ndoa, kitamsaidia kufanya uchaguzi sahihi na kumgundua mwenzi aliye bora.

"Kwa wanandoa ni tiba, kinaboresha na kutibu ndoa zote zilizo ICU. Sijakurupuka kutoa kitabu hiki, nimefanya utafiti kwa miaka mitano, kabla ya kukitoa. Kimethibitishwa na wataalamu mbalimbali akiwemo Mchungaji Michael Kabisa ambaye ni msomi mwenye Shahada ya Kwanza ya Theolojia / Shahada ya Kwanza ya Sosholojia / Shahada ya Kwanza ya Sayansi ya Siasa. Kinawafaa watu wazima wenye umri wa kuanzia miaka 20 na kuendelea. Ni tulizo na jibu la ndoa zote."

*UMESHAANDIKA VITABU VINGAPI MPAKA SASA?*

"Vingi sana. Lakini kwa upande wa vitabu vya mahusiano, hiki ni kitabu cha sita. Vingine ni True Love (Season 1 – 4), Secret Love (Season 1 – 3), Let's Talk About Love, All About Love na Maisha ya Ndoa (Season One) .

"Baadhi ya vitabu vyangu vya riwaya ni Chotara, Wino Mwekundu, Mateka Ughaibuni na Moyo Wangu Unauma."

*UNA MPANGO WA KUTOA VITABU VINGAPI MWAKA HUU?*

"Mwaka jana niliahidi kutoa vitabu 12 (wastani wa kitabu kimoja kila mwezi), lakini niliishia kuchapa vitabu vinne tu. Mwaka huu sikuahidi na ninaogopa kuahidi, lakini kwa mwezi huu – Mei natarajia kutoa vitabu vitatu. Hiki kinatangulia – vingine viwili nitavitambulisha hivi karibuni kwenye tukio kubwa, wadau wasubiri kwa hamu."

*VITABU VYAKO UNACHAPIA WAPI?*

"Kwa muda mrefu nilikuwa nachapiwa na wachapaji tofauti tofauti kwa bei kubwa, lakini kwa sasa nachapa mwenyewe kwa gharama nafuu sana. Ninayo kampuni ya uchapaji, ambayo pia tunapokea kazi za waandishi wengine.

"Bei yetu ni rafiki sana na kazi zetu ni bora. Unapata kazi yako ndani ya muda mfupi sana. Nawakaribisha waandishi wenzangu JOPASHA PRODUCTION tufanye kazi. Hata ukiwa na mtaji wa laki moja tu, kwetu unachapiwa kitabu."

*WASOMAJI WATAKUFIKIAJE?*

"Napatikana sana mitandaoni kwenye kurasa zangu, nikitumia jina la Joseph Shaluwa (Facebook) au kwenye ukurasa wangu wa simulizi za joseph shaluwa (Facebook), @josephshaluwa (Instagram) na @Joseph Shaluwa (Twitter).

"Kazi zangu zinapatikana kwenye Gazeti la Championi Ijumaa, Jarida la Jahazi (kwenye meli na boti za Kilimanjaro – zinazofanya safari za Dar – Unguja – Pemba na Jarida la Twiga – Inflight Magazine, linalopatikana kwenye ndege za Air Tanzania.) Zaidi ni kwenye vitabu vyangu."



**JOSEPH SHALUWA**

*KITABU HIKI KITAPATIKANA VIPI?*

"Kitabu hiki cha Maisha ya Ndoa na vitabu vyangu vingine vinapatikana katika Duka la Kona ya Riwaya – Kinondoni Block 41, Come & Read BookStore – Ununio na Kwa George – Posta Mpya. Mikoani vitabu vinatumwa kwa gharama nafuu. Kwa mawasiliano zaidi, wasomaji wanifuate kwenye kurasa zangu za mitandao ya kijamii kwa ufafanuzi zaidi."

@@@

**MAISHA YA NDOA-TOLEO JIPYA**

**"Kwa wanandoa ni tiba, kinaboresha na kutibu ndoa zote zilizo ICU."**

# Tangazo




**NGURUMO YA MWANDISHI**

**S.L.P 1039**
**IRINGA—TANZANIA**

**Instagram: jamvi la simulizi**

**Email: jamvilasimulizi”gmail.com**

**Whatsapp: 0734550514**

**Mob: 0766974865**
**0672160016**


## NGURUMO YA MWANDISHI— *tu ze neksiti levo*

















**Na: Rey Stanley**

Ni miezi saba sasa Jarida pepe la Ngurumo ya Mwandishi limeendelea kuburudisha, kufundisha, kuelimisha na kuhabarisha. Mapinduzi yaliofanywa na jarida hili si ya kubezwa na yamepata pongezi nyingi kutoka ndani na nje ya nchi. Nasi pia tunakushukuruni nyote kwa kujitoa kwenu kutupatia maandiko mbalimbali bila ya gharama yoyote. Mungu akubarikini sana.

Kutokana na maoni ya wapenzi wa jarida hili, wadau wa masuala ya habari na kumbukumbu za machapisho hapa nchini, wameshauri kuboresha mambo kadhaa ikiwemo kuongeza kurasa na contents na wapenzi wa riwaya wameomba kuongezwa urefu na idadi ya riwaya, na mengine mtakayoyaona hapohapo. Nasi tumeyapokea yote hayo na tunaahidi kuyafanyia kazi polepole kuanzia toleo lijalo. Tunakaribisha makala zinazozungumzia uanishi na fasihi, mashairi na mahapisho anuai yaliyojikita katika ukuzaji na mwendelezo wa fasihi anishi na simulizi kwa ujumla. Wasiliana nasi kwa WhatsApp 0734550514